

Wizara ya Kazi ya Marekani

Matokeo ya Mwaka 2023 Kuhusu Aina Mbaya Zaidi za Ajira kwa Watoto

Tanzania

Mnamo mwaka 2023, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maendeleo ya wastani katika jitihada za kutokomeza aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto. Serikali iliidhinisha na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kitaifa uliosasishwa wa Kutokomeza Ajira kwa Watoto na kufanya tathmini ya kimsingi ya sera na desturi za ajira kwa watoto za makampuni yanayohusika katika mitandao mikuu ya ugavi wa kilimo. Kwa kuongezea, serikali ilifadhili midahalo ya kijamii na kampeni ya televisheni ya ufahamu wa umma juu ya kukabiliana na usafirishaji haramu wa watu. Hata hivyo, mapungufu yamesalia katika mfumo wa kisheria na utekelezaji wa sheria zinazohusiana na ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa adhabu kwa utumiaji wa watoto katika shughuli haramu, ukosefu wa ulinzi wa umri wa chini kwa watoto wanaofanya kazi za majumbani, na idadi isiyotosha ya wakaguzi wa kazi wa kufuatilia nguvu kazi ya Tanzania.

Hatua zilizopendekezwa za serikali hapo chini zingeweza kuziba mapengo ambayo USDOL imetambulisha katika utekelezaji wa Tanzania wa ahadi zake za kimataifa za kuondoa aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto.

Eneo	Hatua Inayopendekezwa
Mfumo wa Kisheria	Panua orodha ya kazi hatarishi na shughuli zilizopigwa marufuku kwa watoto ikiwa ni pamoja na upaliliaji na usindikaji katika uzalishaji wa tumbaku, karafuu, kahawa, mkonge na chai.
	Haramisha matumizi ya watoto katika shughuli haramu, hususani katika uzalishaji na usafirishaji wa madawa ya kulevya.
	Haramisha uandikishaji wa watoto chini ya umri wa miaka 18 unaofanywa na vikundi visivyo vya serikali.
	Eneza ulinzi wa umri wa chini zaidi ili ulinzi huo utumiwe kwa watoto wote, ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya kazi za majumbani.
	Ongeza umri wa elimu ya lazima kutoka umri wa miaka 13 hadi 14 ili kuendana na umri wa chini kabisa wa kufanya kazi.
	Anzisha kwa mujibu wa sheria elimu ya msingi ya umma bila malipo na kuondoa mamlaka ya kisheria ya mamlaka za elimu za mitaa kutathmini ada za elimu ya hiari.
Utekelezaji	Ongeza rasilimali za kibajeti kwa ajili ya utaratibu wa malalamiko ya ajira kwa watoto ili utaratibu huo uweze kutekeleza operesheni zake kikamilifu.

Eneo	Hatua Inayopendekezwa
	<p>Ongeza rasilimali za kifedha na nyenzo, ikiwa ni pamoja na vifaa vya ofisi, usafirishaji, na mafuta, kwa ajili ya ukaguzi wa kazi, na pia ongeza idadi ya wakaguzi wa kazi kutoka 87 hadi 643 ili kuhakikisha ujumuishi wa kutosha wa wafanyikazi wa takriban milioni 25.7.</p> <hr/> <p>Anzisha utaratibu mkuu wa kukusanya na kuchapisha data zinazohusika na desturi mbaya zaidi za ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na idadi ya uchunguzi na kutozwa adhabu kwa ajili ya ukiukaji.</p> <hr/> <p>Hakikisha kwamba idadi ya ukaguzi wa kazi unaofanywa inalingana na ukubwa wa ukaguzi wa kazi ili kudumisha ubora wa kutosha na upeo wa ukaguzi.</p> <hr/> <p>Chapisha taarifa kuhusu juhudi za utekelezaji wa sheria za uhalifu zinazohusiana na aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto, ikiwa ni pamoja na idadi ya uchunguzi, mashtaka na kupatikana na hatia.</p>
Uratibu	<p>Hakikisha kwamba Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Elimu kuhusu Ajira Kwa Watoto kinaweza kutekeleza amri zilizokusudiwa.</p>
Sera za Serikali	<p>Ondosha masharti katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi yanayokatiza watoto ambao hapo awali walifeli mtihani huo wasiurudie kwa ajili ya kuzingatiwa katika kukubaliwa kwenye shule za sekondari.</p>
Mipango ya Kijamii	<p>Wezesha kuandikishwa upya kwa wasichana wanaoacha shule wakati wa ujauzito.</p> <hr/> <p>Fanya elimu ipatikane kwa watoto wote nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na wale wanaoishi vijijini, kwa kuhakikisha rasilimali za kutosha kwa watoto wenye ulemavu na matatizo ya kujifunza; kuongeza rasilimali kwa walimu, madarasa na madawati, chakula, na vifaa vya usafi wa mazingira; na kulipa gharama zisizo rasmi zinazotozwa familia, zikiwemo sare za shule, vitabu na vifaa vingine vya kujifunzia.</p> <hr/> <p>Oanisha hatua za kuzuia na kukomesha ajira kwa watoto na kuziingiza hatua hizo katika Mpango wa Uhawilishaji Fedha Taslimu wenye Masharti wa Mfuko wa Hatua ya Kijamii ili kuongeza ufanisi wake.</p> <hr/> <p>Fanya shughuli za kutekeleza Mpango wa Uhawilishaji Fedha Taslimu wenye Masharti wa Mfuko wa Hatua ya Kijamii Tanzania na pia fanya taarifa kuhusu hatua za utekelezaji zipatikane hadharani.</p> <hr/> <p>Endeleza programu zinazojumuisha watoto wanaoshiriki ajira kwa watoto katika kazi za majumbani, uvuvi na sekta zisizo rasmi.</p>